KISWAHILI

Tarehe: 05 / 07 /2022
Wakati: 8h30' -10:30'

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

KIWANGO: **Kidato cha Tano**
MICHEPUO **Somo la kuchaguliwa**

MUDA: **Saa mbili (2)**

ALAMA: **..... /40**

MAELEKEZO

- Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
- Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne: Ufahamu, Sarufi, Fasihi na Utungaji.
- Mtihani huu unaundwa na maswali 10.
- Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.
- Tumia kalamu ya bluu au nyeusi

SEHEMU YA I: UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kuhusu mchezo wa kandanda, halafu jibu maswali uliyopewa hapo chini.

Katika Afrika hivi leo kuna baadhi ya watu wa kawaida ambao hujiuliza jinsi gani mazao ya biashara kama mkonge, korosho, tumbaku, kahawa,... huwasaidia iwapo mazao hayo huuzwa katika nchi za ng'ambo.

Swali hili huzushwa na msisitizo wa viongozi wengi kwamba wananchi walime mazao hayo ili kuweza kupata fedha za kigeni. Kitu ambacho wananchi hawa hawakielewi ni vipi fedha za kigeni hufanya kazi kubwa ya kuinua maendeleo ya nchi. Wengi wao hawajui kwamba hata vitu ambavyo hutumiwa katika maisha ya kila siku huhitaji fedha za kigeni kununuliwa kutoka nchi za kigeni. (Hapa fedha za kigeni maana yake ni zile fedha ambazo kimataifa zinakubalika kufanyia biashara, mathalani dola, yen na kadhalika). Tuchukue mfano wa nyembe za kunyolea. Nchini Rwanda nyembe hizo huagizwa kutoka Ufaransa na nchi nyingine. Lakini kitu kama nyembe ni watu wachache wanaoweza kufikiria kwamba huhitaji dola au faranga za Ufaransa kuweza kununuliwa kutoka nchi za nje.

Hata bidhaa ambazo huzalishwa nchini Rwanda nazo zina uhusiano wa moja kwa moja na fedha za kigeni. Tuchukue mfano wa kiwanda cha bidhaa za plastiki kilichoko jijini Kigali. Ili kiwanda hiki kiweze kufanya kazi barabara, ni lazima baadhi ya malighafi iagizwe kutoka nchi za nje. Rwanda haina viwanda-mama vya kuzalisha mitambo. Hivyo, mitambo nayo huagizwa kutoka nchi za nje.

Hivi, ndiyo kusema kuwa msisitizo wa kuzalisha mazao ya biashara unaofanywa na viongozi wengi ni wa msingi. Ni jukumu la viongozi kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili ili wanapofanya shughuli ya uzalishaji wa mazao ya biashara waelewe umuhimu wake kwa taifa. Ni kwa kufanya hivi tu: Wananchi watazalisha mali wakiwa na mwamko na hatimaye kuweza kuongeza kiwango cha uzalishaji.
Kadiri bidhaa zitakavyoongezeka, ndivyo mapato ya fedha za kigeni yatakavyokua, na ndivyo nchi itakavyostawi kiuchumi. Matokeo yake ni maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Maswali ya Ufahamu

1. Mazao yanayouzwa katika nchi za ng'ambo yanasaidia nini wananchi? **(alama 4)**
2. Toaa mfano wa bidhaa ambayo huagizwa kutoka nchi za kigeni **(alama 3)**
3. Toa maana ya fedha za kigeni **(alama 3**)

4. Katika mistari kati ya 5 na 7, toa muhtasari wa kifungu hiki ulichokisoma **(alama 5)**

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 10)

5. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia neno sahihi kati ya haya: **umuhimu, ufukara, rahisi ufasaha, inashughulikia, kiutandawazi, , husika. (Alama 4)**

a) Nadharia ya ..... ni mojawapo kati ya nadharia zinazohusu kueleza chanzo, ukuaji na ueneaji wa fasihi simulizi.
b) Serikali ya Rwanda huhamasisha raia kuhusu..... wa amani na maendeleo ya kudumu.
c) .....wa lugha huwasaidia viongozi mbalimbali kuaminiwa na raia kuhusu mikakati iliyochukiliwa na serikali zao.
d) ..... unaendelea kupigwa marufuku nchi Rwanda kutokana na sera thabiti za serikali.
e) Maswali yote ya mtihani yalikuwa .....

6. Weka sentensi zifuatazo katika hali kanushi: **(alama 2)**

a. Kabanda anaandaa meza
b. Wanafunzi wote wamemaliza kufanya jaribio

7. Tunga sentensi moja kwa kila aina ya sentensi zifuatazo: **(Alama 3)**

a) Sentensi sahili
b) Sentensi ambatano
c) Sentensi shurutia

SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 5)

8. Fasihi ni nini? **(Alama 2)**

9. Tunga sentensi kwa kutumia nahau zifuatazo: **(alama 3)**

a. Kupiga umaridadi
b. Kula chumvi nyingi
c. Kuvaa miwani

SEHEMU YA IV : UTUNGAJI (Alama 10)

10. Chagua mada moja itunge insha yenye maneno kati ya 100 na 120.: **(alama 10)**

a. Mchango wa vijana katika maendeleo ya nchi
b. Athari za kuavya mimba
c. Elimu ndio msingi wa maendeleo

MWISHO!

KISWAHILI

Tarehe: 22 / 06 /2022
Wakati: 8h30' am-11:30' am

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

KIWANGO: **Kidato cha Tano**
MICHEPUO **LKK, LKF**

MUDA: **Saa tatu (3)**

ALAMA: **..... /100**

MAELEKEZO

- Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
- Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne: Ufahamu, Sarufi, Fasihi na Utungaji.
- Mtihani huu unaundwa na maswali 20.
- Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.
- Tumia kalamu ya bluu au nyeusi

MTIHANI WA KUMALIZA MWAKA 2021-2022

Kidato cha Tano

Mchepuo wa Lugha

Mwaka wa shule: 2021-2022

Muda: Saa 3

Jumla ya alama: 100

SEHEMU YA I: UFAHAMU (alama 25)

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali yanayohusika

Jongoo na chura

Hapo zamani palitokea Jongoo na Chura ambao walikuwa marafiki wakubwa sana. Kila wakati walikuwa wanatembeleana.
Siku moja, Chura alimwuliza Jongoo, "Rafiki yangu huwa unafanya nini na ngozi yako? Mbona inang'ara sana! Tazama ngozi yangu, siyo laini. Ningependa iwe kama yako. Hebu nidokezee kidogo".

Jongoo alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo. Alianza kumpa rafiki yake ushauri kama ifuatavyo, "rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa tena ngumu ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango kwenye moto kisha hujaza mafuta...". Kabla hajaendelea na kumaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake kwa kusema, "Basi! Basi! Nimeisha elewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote haya nitayatenda na utaona nitakavyonawiri".

Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule amekwisha elewa kila kitu. Marafiki wale waliagana. Alipofika nyumbani Chura, alimwita mkewe na kumwambia, "Mke wangu! Leo rafiki yangu Jongoo amenieleza jinsi ya kuifanya ngozi yangu iwe nyororo na ya kung'ara kama yake. Sasa hivi ninataka uweke chungu jikoni. Hakikisha jiko lina moto mkali sana".

Mke alifanya kama alivyoelezwa. Chura aliendelea kutoa maagizo, "Ninataka utie mafuta ya kukaangia mboga mengi sana. Yakiisha chemka unieleze mara moja". Mkewe alitekeleza maagizo ya mara kwa mara na kumpa taarifa kwamba mafuta yalikwisha kuchemka. Chura aliingia jikoni akamwambia mkewe, "sasa nitumbukize katika mafuta maana ninataka niibabue ngozi hii ya juu ili ibaki

nyororo iliyopo chini yake". Mkewe alipigwa na bumbuazi na kumjibu, "Mume wangu, mbona unaniambia nifanye kitu cha hatari! Ukitumbukizwa katika mafuta haya utapona? Haiwezekani hata kidogo! Balaa hilo!"

Chura alisisitizia kwa ukali kutumbukizwa katika mafuta. Alisema, "Mimi nilikuwa nikikuambia siku zote kwamba ngozi hii inanitia aibu na leo nimepata njia ya kuiondoa, na wewe unapinga! Ukitaka kukaa nyumbani kwangu sharti utimize ninayokuambia kufanya ama sivyo nitakufukuza!"

Mkewe Chura kusikia hivyo, alimnyanyua mumewe na kumtumbukiza katika kikaango. Chura alilia, "Yooooo! Yooooo! Nigeuze upande mwingine!" Mkewe alipomgeuza tu mlipuko mkubwa ulisikika. Chura alipasuka vipande. Utumbo ulitoka katika kikaango na kuanguka chini. Huu ndio ulikuwa mwisho wa mzee Chura.

Mauti ya kujitakia yalimfikia. Mkewe alipoona yaliyokuwa yametokea, alikimbia mara moja na kuwaita majirani. Majirani walikuja kushuhudia msiba. Mjane aliwaelezea jinsi alivyoshurutishwa kumtumbukiza marehemu katika mafuta. Majirani waliamua kwamba mke hakuwa na hatia bali marehemu Chura alisababisha kifo chake mwenyewe kwa ujinga wake.
Huu ndio mwisho wa hadithi!

Jibu maswali yafuatayo kuhusu kifungu cha habari kilicho hapa juu (alama 25)

1. Taja majina ya wahusika wanaozungumziwa **(alama 2)**

2. Thibitisha kwamba Jongoo na Chura walikuwa marafiki **(alama 3)**
3. Unafikiri ni kwa sababu gani Chura alimkataza rafiki yake Jongoo kumaliza ushauri aliompa? **(alama 3)**
4. Kwa maoni yako, matarajio ya Chura kuhusu ushauri wa Jongoo yalikuwa yapi? **(alama 4)**
5. Ni kwa sababu gani Mkewe Chura alipigwa na bumbuazi? **(alama 4)**
6. Ni kwa sababu gani Chura alikuwa anataka kuiondoa ngozi yake? **(alama 2)**
7. Ilikuwaje mke wa Chura alipomweka katika mfuta? **(alama 3)**
8. Majirani walipokeaje kifo cha Chura? **(alama 4)**

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 25)

9. Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo: **(alama 5)**
   a. Laini
   b. Haja
   c. Hatari
   d. Bumbuazi

e. Kushuhudia

10. Andika sentensi zifuatazo katika umoja: **(Alama 8)**

a. Majambazi waliiba na kuua watu usiku
b. Wezi walikamatwa na polisi
c. Maji yamemwajika chini
d. Mawe yalitupwa katika maji

11. Tunga sentensi moja kwa kila aina ya tungo za Kiswahili zifuatazo: **(Alama 6)**

a. Tungo sahili
b. Tungo ambatano
c. Tungo shurutia

12. Taja njia mbili za uchanganuzi wa sentensi. **(Alama 2)**

13. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya maneno: **(Alama 4)**

- Mtoto huyu alichelewa jana.

SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 30)

14. Katika kifungu cha habari ulichokisoma hapo juu:

a. Taja majina ya wahusika wakuu na kueleza sababu za kuwaita wahusika wakubwa **(alama 2.5)**
b. Taja majina ya wahusika wasaidizi na kueleza sababu za kuwaita wahusika wadogo **(alama 2.5)**

15. Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiri na kukumbuka. Eleza kauli hii. **(Alama 5)**

16. Jaza methali zifuatazo: **(Alama 5)**

a. Angurumapo ……mcheza nani.
b. Usitukane ……..na uzazi ungalipo.
c. Mwezi na……giza na mwizi.
d. Mtaka yote kwa ……..hukosa yote.
e. Dalili ya mvua …….

17. Tegua vitendawili vifuatavyo: **(Alama 5)**

a. Yeye anasuka mikeka lakini hulala chini.
b. Saa yangu kila siku hutembea, ikisimama haitengenezeki tena.
c. Anajipiga kisha Analia.
d. Hazikauki umande.
e. Nyumba yangu haina mlango.

18. Toa maana ya nahau na misemo hii: **(Alama 5)**

a. Kugonga mwamba
b. Kuwa na damu ya kunguni
c. Kuchapa maneno
d. Kulea mtoto kwa hali na mali
e. Mtu mwenye domo kaya

19. Tumia nahau zifuatazo katika sentensi. **(Alama 5)**

a. Kuvaa miwani
b. Kupiga umaridadi
c. Kula chumvi nyingi
d. Kumwaga unga
e. Kutia jeki

SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 20)

20.

a. Nini maana ya risala? **(Alama 2)**
b. Taja sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi. **(Alama 3)**
c. Tunga insha yenye maneno kati ya 200 na 250 kuhusu mada ifuatayo: **(Alama 15)**

"Ndege aamukaye mapema hula wadudu watamu".

MWISHO!

MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA KUMALIZA MWAKA 2021-2022

Kidato cha Tano

Michepuo mingine

Mwaka wa shule: 2021-2022

Muda: Saa 2

Jumla ya alama: 40

SEHEMU YA KWANZA: UFAHAMU (alama 15)

1. Yanawasaidia kupata fedha za kigeni
2. Nyembe
3. Ni zile fedha ambazo kimataifa zinakubalika kufanyia biashara, kama vile dola, yen na kadhalika
4. Muhtasara unaotungwa uwe na maana, matumizi ya lugha sahihi, matumizi ya lugha kibinafsi pasipo kunakili maneno na sentensi kama vilivyo katika kifungu cha habari

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 10)

5. Kukamilisha sentensi **(Alama 4)**
   a. Kiutandawazi
   b. Umuhimu
   c. Ufasaha
   d. Ufukara
   e. Rahisi

6. Hali kanushi

a. Kabanda haandai meza
b. Wanafunzi wote hawajamaliza jaribio

7. Mifano ya sentensi **(Alama 5)**
   a. Barua ni nusu ya kuonana.
   b. Mwalimu anafundisha na wanafunzi wanamsikiliza.
   c. Ukiomba utapewa.

SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 5)

8. Fasihi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala mbalimbali yanayomhusu binadamu. Au fasihi ni kazi ya sanaa imulikayo hisi mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha. **(Alama 3)**

9. Mifano :

a. Katika ndoa ya Kalisa alikuwa amepiga umaridadi
b. Babu yake Muhire amekula chumvi nyingi. Sasa ana miaka 100

c. Katika sikukuu ya ubatizo wa kaka yangu watu wengi walikunywa pombe nyingi na kuvaa miwani

SEHEMU YA IV : UTUNGAJI (Alama 10)

10.
Wakati wa kutunga Insha ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo:

- Sarufi/matumizi ya lugha sahihi
- Usafi wa maandishi
- Mgawanyiko wa aya
- Mtiririko wa mawazo yenye mantiki
- Mpangilio na mwonekano mzuri wa insha

SEHEMU KUU ZA INSHA

1. **Mada** au **kichwa cha insha**: Mada ya insha hutambulisha jambo linalozungumziwa katika insha. Mada ya insha haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Lazima mada iwe na mvuto kwa msomaji.

2. **Utangulizi** au **mwanzo wa insha**: Utangulizi wa insha mara nyingi huwa ni aya moja tu. Unafaa kuvutia kwa kiwango cha juu ili kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma insha nzima. Katika sehemu hii inampasa mwandishi atoe maelezo mafupi na maana ya habari aliyopewa

3. **Kiini cha insha**: Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa insha nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha. Inamlazimu mwandishi afafanue kwa mapana mada anayoishughulikia huku akitoa mifano hai inayoendana na hali halisi. Kwa kawaida sehemu hii hueleza kwa ukamilifu kila hoja iliyodokezwa katika utangulizi.

4. **Hitimisho** au **mwisho wa insha:** Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyoandikwa katika mwili wa insha kwa namna ya kuvutia msomaji. Inampasa mwandishi kutoa mapendekezo (maoni) ya msingi au kusisitiza kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika habari yenyewe. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili.

MWISHO!

MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA KUMALIZA MWAKA 2021-2022

Kidato cha Tano

Mchepuo wa Lugha

Mwaka wa shule: 2021-2022

Muda: Saa 3

Jumla ya alama: 100

SEHEMU YA I: UFAHAMU (alama 25)

1. Ni Chura, Mke wa Chura, Jongoo, majirani wa familia ya Chura
2. Jongoo na Chura walikuwa wanatembeleana kila wakati na kupeana maadili
3. Ni kwa sababu Chura alikuwa anadhani ameishajieleza yatakayofuata
4. Matarajio ya ushauri wa Jongoo kwa Chura yalikuwa kuweka mafuta katika kikaango, kuyaweka kwenye moto mpaka yakachemka na kujiweka katika mafuta hayo kwa ajili ya kuwa na ngozi laini kama ya Jongoo
5. Ni kwa sababu ya maagizo aliyopewa na mme wake Chura ya kumweka katika mafuta yaliyochemka. Mke wa chura aliona kwamba maagizo ya Chura yanaweza kusababisha kifo.
6. Ni kwa sababu ngozi yake ilikuwa inamtia aibu kwani haikuwa laini wala nyororo
7. Ngozi ya Chura iliungua, akapasuka vipande, utumbo wake ukaangukia chini na kufa papo hapo
8. Majirani waliona kwamba marehemu Chura ndiye aliyejiletea kifo kwa kumshurutisha mke wake kumweka katika mafuta yaliyochamka

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 25)

9. **Mifano:**

a. Mwili wangu ni laini kama wa mtoto mdogo
b. Sina haja ya kwenga sokoni
c. Alijitia hatarini alipowachokoza nyuki
d. Mama alishikwa na bumbuazi aliposikia mtoto wake alifanya ajali
e. Watu wengi walikuja kushuhudia mashindano ya mpira wa miguu

10. Umoja wa sentensi

a. Jambazi aliiba na kuua mtu usiku

b. Mwizi alikamatwa na polisi

c. Maji yamemwajika chini
d. Jiwe lilitupwa katika maji

11. Mifano ya tungo:

a) Mwanafunzi anasoma kitabu.
b) Watoto wanacheza na wanaimba nyimbo.
c) Ningejifunza vizuri ningepata alama nzuri.

12.

Njia za uchanganuzi wa sentensi: **(Alama 2)**
Njia ya mishale au mistari;
Njia ya visanduku au ya jedwali;
Njia ya matawi;
Njia ya maneno.

13. Kuchanganua sentensi kwa njia ya maneno: **(Alama 4)**

Mtoto huyu alichelewa jana.
N V T E

SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 30)

14.

a. Wahusika wakuu ni Chura na Jongoo kwa sababu ndio wanaoendeleza hadithi kutoka mwanzo hadi mwisho. Wahusika hawa ndio kiindi cha hadithi
b. Wahusika wasaidizi ni mke wa Chura na majirani wa familia ya chura kwa sababu walisaidia kumjenga mhusika mkuu Chura

15. Kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu mazingira yake na kujaribu kupata jibu. Katika shughuli hii, mteguzi huwaza sana kuhusu mazingira hayo na kulinganisha majibu mbalimbali yanayoweza kutolewa. Hii ni namna moja ya kukuza uwezo wake wa kukumbuka na kufikiri. **(Alama 5)**

16. Jaza methali zifuatazo ili ziwe kamili. **(Alama 5)**

a) Angurumapo simba, mchezaji nani;
b) Usitukane wakunga na uzazi ungalipo;
c) Mwezi na mtembezi, giza na mwizi;
d) Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.
e) Dalili ya mvua ni mawingu

17. Vitendawili (Alama 5)

a. Yeye anasuka mikeka lakini hulala chini: **Boga**
b. Saa yangu kila siku hutembea, ikisimama haitengenezeki tena: **Moyo**

c. Anajipiga kisha analia: **Jogoo**
d. Hazikauki umande: **Pua za mbwa**
e. Nyumba yangu haina mlango**: Yai**

18. Misemo na maana zake **(Alama 5)**

a. Kugonga mwamba = Kutofanikiwa
b. Kuwa na damu ya kunguni = Kuwa na tabia mbaya
c. Kuchapa maneno = Kubuni maneno ya uongo juu ya mtu
d. Kulea mtoto kwa hali na mali = Kulea mtoto vizuri uwezavyo
e. Mtu mwenye domo kaya = Mpayukaji ambaye hawezi kutunza siri

19. Tumia nahau zifuatazo katika sentensi. **(Alama 5)**

a. **Kuvaa miwani**: Mugeni alivaa miwani kutokana na pombe nyingi.
b. **Kupiga umaridadi**: Kagabo alipoenda kanisani alikuwa amepiga umaridadi.
c. **Kula chumvi nyingi**: Mzee yule amekula chumvi nyingi.
d. **Kumwaga unga**: Kwa sababu ya ulevi, Mutoni alimwaga unga akakosa la kufanya.
e. **Kutia jeki:** Alipohisi kwamba ameanza kuishiwa na nguvu walimtia jeki na kuendelea na safari.

SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 20)

20.

a. Risala ni taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani aghalabu inayoeleza haja inayotakiwa.**(Alama 2)**
b. Sababu nne zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi ni kama vile kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, kuandikia meneja wa gazeti na kadhalika. **(Alama 4)**
c. **Hoja: (Alama 15)**

- Kuamka mapema
- Kufanya kazi kwa bidii
- Kupenda kazi
- Kutokata tamaa
- Kufanikiwa kutokana na kazi uliyoifanya
- Kujilinda uvivu na uzembe

Wakati wa kutunga Insha ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo:

- Sarufi/matumizi ya lugha sahihi
- Usafi wa maandishi
- Mgawanyiko wa aya
- Mtiririko wa mawazo yenye mantiki
- Mpangilio na mwonekano mzuri wa insha

SEHEMU KUU ZA INSHA

1. **Mada** au **kichwa cha insha**: Mada ya insha hutambulisha jambo linalozungumziwa katika insha. Mada ya insha haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Lazima mada iwe na mvuto kwa msomaji.

2. **Utangulizi** au **mwanzo wa insha**: Utangulizi wa insha mara nyingi huwa ni aya moja tu. Unafaa kuvutia kwa kiwango cha juu ili kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma insha nzima. Katika sehemu hii inampasa mwandishi atoe maelezo mafupi na maana ya habari aliyopewa

3. **Kiini cha insha**: Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa insha nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha. Inamlazimu mwandishi afafanue kwa mapana mada anayoishughulikia huku akitoa mifano hai inayoendana na hali halisi. Kwa kawaida sehemu hii hueleza kwa ukamilifu kila hoja iliyodokezwa katika utangulizi.

4. **Hitimisho** au **mwisho wa insha:** Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyoandikwa katika mwili wa insha kwa namna ya kuvutia msomaji. Inampasa mwandishi kutoa mapendekezo (maoni) ya msingi au kusisitiza kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika habari yenyewe. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili.

MWISHO !